

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam.
Tarehe 11 Machi 2006**

Waliohudhuria

Devidi Ludago

Elaine Baker

Ibrahim Kizyara

Israel Kiyame

Juma Ali Salehe Jongo

Mejah Mbuya

Pitra Andrea

Selemani Almasi

Sosthenes C. Amlima

Wanachama wapya

Wanachama wawili waliohudhuria mkutano huu. Sosthenes alitambua yeye ni msanii na amefanya kazi katika mashirika yanayojihusisha na UKIMWI. Pitra alitambua anatokea Kigamboni na anatumia baiskeli ya mkono kama usafirikwani ni mlemavu.

Usajili

Mejah alitufahamisha kuwa UWABA imefanikiwa kusajiliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Matangazo

Elaine na Juma walipeleka matangazo kwenye ofisi nyingi za magazeti Dar es Salaam jumamosi tarehe 4 machi. Meja alifuatilia jambo hili na kufanikiwa kusailiwa na Sunday Citizen-na makala hiyo itatolewa jumapili. Magazeti ya Majira na Daily Times pia walisema watayatoa matangazo yetu

Barua ya Utambuzi

Mejah aliandaa idadi ya maskirika ambayo UWABA itajitambulisha kwayo, wajumbe wengine waliongeza. Mashirika hayo ni kama yafuatavyo:

Serikali

- Wizara ya Mawasiliano na Miundo mbinu
- Wakala wa barabara(TANROAD)
- Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam
- Halmashauri ya wilaya ya Ilala
- Halmashauri ya wilaya ya Temeke
- Halmashauri ya wilaya ya Kinondoni
- Askari wa usalama wa barabarani
- SUMATRA-mamlaka ya usafiri wa daladala
- Wizara ya Elimu-kuhusu usalama wa usafiri wa baiskeli kwa watoto kwenda shuleni
- Rais Kikwete

Mashirika yasiyo ya kiserikali

- Muungano wa mashirika yasiyo ya kiserikali (TANGO)
- Baraza la taifa la Mazingira
- Chama cha waandishi wa habari Wanawake Tanzania
- Kitua cha sheria na Haki za Binadamu

Mashirika ya kibiashara

- Kampuni ya Taifa ya kutengeneza baiskeli (NABICO)
- GUTA karibu na Tazara inayotengeneza baiskeli za tairi tatu (GUTA)
- Kampuni ya utengenezaji wa tairi za Baiskeli, Bora karibu na Mwenge
- Kampuni za china na Bakresa zinazotumia baiskeli katika uuzaji wa icecream (majina kutafutwa)
- Kampuni ya Vodacom itumiayo baiskeli kwa walemavu kuuza vocha za simu.
- Kampuni za Ulinzi zitumiazo baiskeli- Dragon, Ultimate Security, Net Support Group 4.
- Makampuni makubwa yanayotoa ufadhili, kama vile CRDB, Standard Chartered.
- Wauzaji wa maua wanaotumia baiskeli.

Balozi

- Netherlands (wana maelezo mengi yahasuyo upandaji baisikeli)
- China (waingizaji wakuu wa baiskeli)

Taasisi za Elimu

- VETA (mamlaka ya ufundi stadi) inayofundisha kozi za ukarabati wa baiskeli)
- Kitengo cha Sheria Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Kitengo cha Uhandisi wa barabara chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Ilikubalika kuwa mtazamo wetu uwe kwenye Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi. Mejah aliripoti kuwa amepeleka barua za utambuzi na ameandaa babua za kuomba kukutana. Kwenye mkutano nia yetu kuu itakua kuangalia jinsi gain UWABA imeshiriki katika mchakato wa upangaji wa barabara.

Jukwaa la Jamii Tanzania

Jukwaa hili limeandaliwa kufanywa tarehe 22 hadi 25 Machi Mmoja. Ilikubalika kuwa UWABA itakuwa na banda hapo. Mejah alisema kuwa atafuatilia maelezo zaidi kwa waandaji wa jukwaa, TANGO.

Mtandao wa kimataifa

Elaine aliripoti kuwa amefanikiwa kuitambulisha UWABA kwenye PABIN (mtandao wa habari kuhusu baiskeli) kupitia kupitia orodha ya barua pepe AfriBikeNet. Alijibiwa na Ibike na kutoka kampuni ya ushauri ya Ujerumani inayofanya utafiti kuhusu mambo mbalimbali ya baiskeli kwa ajili ya mipango barabara.

Mpango kazi

Elaine aliodhoresha vigezo ambavyo eneo la kazi lingehitajika kuwa navyo ili kupata cheti cha eneo litakalofaa kwa matumizi ya baiskeli kutoka UWABA.

Mashindano ya insha

Israeli aliripoti kuwa ndugu yake amejiunga na mashindano ya insha ya baiskeli.

Harambee

Israeli alipendekeza kuwa kamati ndogo ya harambee iundwe.

Kukuza matumizi ya baiskeli

Mawazo kuhusu jinsi ya kukuza matumizi ya baiskeli yalijadiliwa.

Kuwe kozi kwa watoto jinsi ya kutunza baiskeli

Kuhamasisha biashara ya baiskeli za kukodi.

Hii itasaidiwa na benki ya Vijana inayoshughulika na mtaji midogo ya mitaji midogo ya miradi kwa vijana ambapo Israeli anahusika.

Nembo

Ilijadiliwa kuwa nembo inahitajika ili kutengeneza vitu mbalimbali vya UWABA. Mejah, Sostenes na Israeli walikubali kuandaa nembo.

Vipeperushi

Elaine alisambaza vipeperushi zaidi vya mkutano.